



The Anglican Diocese of  
Tanga.Church  
St. Augustine Muheza Designated  
District Hospital  
Box 308  
Muheza  
Tanga Region  
Tanzania  
E-mail: office@teule.or.tz  
Fax 2644121

02/08/2021

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI KATIKA HOSPITALI TEULE YA MT.AUGUSTINO WILAYA YA MUHEZA.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali Teule ya Mt. Augustino ya Wilaya ya Muheza amepokea Kibali cha Ajira Mbadala cha kuajiri nafasi **02** za Ajira ya Kudumu za *Daktari Daraja la II nafasi moja (1)* na *Fundi Sanifu Msaidizi Vifaa Tiba* kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora chenye *Kumb. Na FA.10/128/01''I''/132* cha tarehe *19/07/2021* hivyo anawatangazia Watanzania wote wenye sifa kuomba nafasi ya kazi.

### DAKTARI DARAJA LA II (NAFASI 01)

#### 1. Sifa za Muombaji

- 1.1. Awe na Shahada ya Udaktari (Degree of Medicine) kutoka Vyuo Vikuu/Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali.
- 1.2. Awe amemaliza "Internship" na kupata usajili kutoka Baraza la Madaktari Tanganyika (Medical Council of Tanganyika).
- 1.3. Awe na Elimu ya Kidato cha Nne (Form IV) au Kidato cha Sita (Form VI).
- 1.4. Awe na umri usiozidi miaka 45.

#### Kazi na Majukumu ya Daktari Daraja la II

- (a) Kufanya kazi zote za matibabu hospitalini zinazohusiana na magonjwa mbalimbali yakiwemo magonjwa ya watoto, magonjwa ya akina mama na upasuaji wa kawaida na wa dharura.
- (b) Kutoa na kusimamia elimu ya afya pamoja na kuboresha afya ya jamii katika Wilaya na Mikoa au eneo lake la kazi.
- (c) Kuchunguza, kufuatilia na kuzuia milipuko ya magonjwa.

- (d) Kutunza takwimu na kuzitumia kama inavyoelekezwa katika misingi ya MTUHA.
- (e) Kupanga na kutathimini huduma za afya katika eneo lake la kazi.
- (f) Kufundisha wanafunzi na watumishi waliopo kwenye eneo la kazi.
- (g) Kusimamia na kuelekeza wafanyakazi waliopo chini yake.
- (h) Kufundisha wanafunzi katika vyuo vya afya vilivyopo katika eneo lake la kazi.
- (i) Kubuni na kuendesha utafiti na kusambaza matokeo.
- (j) Kubuni na kutayarisha mikakati ya kuinua ubora wa huduma ya fani yake.
- (k) Kuandaa mipango na makisio ya bajeti ya huduma za afya.
- (l) Kushiriki, kuhakiki na kuboresha huduma za afya (medical audit and quality improvement)
- (m) Kutoa huduma za outreach katika Wilaya/Mkoa wake.
- (n) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

### **Ngazi ya Mshahara**

Ngazi ya Mshahara wa Cheo cha Daktari Daraja la II ni **TGHS E.1** yani **Tzs. 1,480,000/=** kwa mwezi.

## **FUNDI SANIFU MSAIDIZI VIFAA TIBA (NAFASI 01)**

### **1.Sifa za Muombaji**

- 1.1. Awe na Cheti cha Ufundi Daraja la II (Vifaa Tiba) kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.
- 1.2. Awe na Elimu ya Kidato cha Nne (Form IV) au Kidato cha Sita (Form VI).
- 1.3. Awe na umri usiozidi miaka 45.

### **Kazi na Majukumu ya Fundi Sanifu Msaidizi Vifaa Tiba**

- (a) Kufanya matengenezo ya vifaa vidogovidogo vya kutolea huduma za tiba kama, "Stethoscope, BP Machine, Sterilizer na Weighing scale".
- (b) Kufanya matengenezo kinga (Preventive Maintenance) ya vifaa katika kituo chake cha kazi.
- (c) Kutunza kumbukumbu za kila siku.
- (d) Kuweka kumbukumbu za vifaa vyote katika eneo lake la kazi.
- (e) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi.

### **Ngazi ya Mshahara**

Ngazi ya Mshahara wa Cheo cha Fundi Sanifu Msaidizi Vifaa Tiba ni **TGHS A.1** yani Tzs. **432,000/=** kwa mwezi.

## 2. MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE;

- (a) Muombaji awe Mtanzania
- (b) Asiwe amewahi kutiwa hatiani kwa kosa la jinai.
- (c) Asiwe amewahi kufukuzwa kazi Serikalini.
- (d) Maombi yote yaambatanishwe na maelezo binafsi ya mwombaji ( CV) na wadhamini wawili na namba zao za simu.
- (e) Maombi ya yaambatanishwe na vivuli vya vyeti vya kuhitimu Taaluma husika na Cheti cha Kidato cha Nne/Sita.
- (f) Waombaji wote wanatakiwa kuwa na vyeti vya kuzaliwa.
- (g) Maombi yawe na Anuani kamili pamoja na Namba za simu ili kurahisisha mawasiliano.
- (h) Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **20/08/2021 saa 9: 30 ALASIRI.**
- (i) Waombaji wenye sifa wataitwa kwenye Usaili.
- (j) Kwa waombaji waliokuwa kazini maombi yao LAZIMA yapitie kwa Waajiri wao.

Maombi yote yatumwe kwa:

**MGANGA MFAWIDHI,**

**HOSPITALI TEULE YA MT AUGUSTINO (W) MUHEZA,**

**S.L.P 308.**

**MUHEZA.**

